TANGAZO LA SERIKALI NA. 784 la tarehe 3/11/2023

SHERIA YA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MAREKEBISHO YA AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA MRADI WA UANZISHWAJI WA KIWANDA CHA UZALISHAJI WA GYPSUM PLASTER NA GYPSUM PLASTER BOARDS KWA KAMPUNI YA KNAUF GYPSUM TANZANIA YA MWAKA 2023

Jina

TS. Na. 654 La 2023

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Marekebisho ya Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Mradi wa Uanzishwaji wa Kiwanda cha Uzalishaji wa Gypsum Plaster na Gypsum Plaster Boards kwa Kampuni ya Knauf Gypsum Tanzania ya Mwaka 2023 na itasomwa pamoja na Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Mradi wa Uanzishwaji wa Kiwanda cha Uzalishaji wa Gypsum Plaster na Gypsum Plaster Boards kwa Kampuni ya Knauf Gypsum Tanzania ya Mwaka 2023 ambayo katika Amri hii itajulikana kama "Amri kuu".

Marekebisho ya Jedwali

2. Amri kuu inarekebishwa katika Jedwali kwa-
(a) kufuta kipimo cha "Kg" katika safu za nne za vipengele vya 589 na 590 mtawalia na badala yake kuweka kipimo cha "Tani"; na
(b) kuongeza tarakimu "7,500" katika safu za tano za vipengele vya 589 na 590 mtawalia.

Dodoma,
19 Octoba, 2023

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*